Stanbic Bank

# MAELEZO NA MASHARTI YA AKAUNTI YA HIFADHI YA MKATABA

## 1. UTANGULIZI

a. Masharti haya yanaanza kutumika unapofungua na kuweka fedha kwa kipindi cha kila mwezi, kwa njia ya agizo la utoaji na sisi katika akaunti ya Hifadhi ya Mkataba.

b. Ni lazima usome, uelewe, na utii Sheria na Masharti haya kwa kuwa ni makubaliano ya lazima kati yako na sisi.

## 2. TAFSIRI

a. Akaunti ina maana ya Akaunti ya Hifadhi ambayo tumefungua kwa jina lako.

b. Tarehe ya Kufungua Akaunti ina maana ya tarehe ambayo Akaunti yako inachukuliwa na sisi kufunguliwa au kuwa hai wakati fedha zinapolipwa, kushughulikiwa na kuonekana katika Akaunti kwa njia ya Agizo la Amana na/au Agizo la kutoa Kima.

c. Siku ya Kazi ina maana ya siku ya kalenda isipokuwa Jumapili na Sikukuu katika Jamhuri ya Muunganio wa Tanzania.

d. Mtaji ina maana ya Kiasi cha Amana na Agizo la Utoaji kilicholipwa na wewe na kupokelewa na sisi katika Akaunti katika Kipindi cha Uwekezaji.

e. Tarehe ya Uanzaji ina maana ya tarehe ambayo kiasi cha mtaji cha kwanza (ikiwa ni kiasi kinachoelezwa nyuma ya fomu ya maombi iliyoandikwa kwa: " Kiasi cha Mtaji wa Awali) kinapokelewa katika Akaunti na itakuwa tarehe ambayo Kipindi cha Uwekezaji kinaanza, bila kuathiri Tarehe ya Ufunguaji Akaunti.

f. Akaunti ya Utoaji ina maana ya Akaunti ya benki uliyoichagua katika hatua ya maombi au baadaye, kuwa ni akaunti uliyoieleza nyuma ya fomu ya maombi iliyoandikwa kama "Akaunti ya Utoaji".

g. Kima cha Agizo la Utoaji ina maana ya kima ambacho umeidhinisha kukitoa kwa mwezi kutoka Akaunti ya Utoaji na kulipa katika Akaunti katika kipindi cha Uwekezaji, na hakihusishi Amana.

h. Tarehe ya Agizo la Utoaji ina maana ya tarehe ambayo umekubali ambayo Kima cha Agizo la Utoaji kinaweza kutolewa katika Akaunti ya Utoaji yako kila mwezi. Ikiwa Tarehe ya Agizo la Utoaji haiangukii katika Siku ya Kazi, Agizo la Utoaji litafanyika Siku ya kazi ifuatayo.

i. Mamlaka ya Agizo la Utoaji ina maana ya ruhusa ambayo umeitoa kwetu kutoa kiautomatiki kima cha Agizo la Utoaji kutoka Akaunti ya Utoaji.

j. Amana ina maana ya kima ambacho unaweza kuweka katika Akaunti, kutoka Tarehe ya Ufunguaji wa Akaunti, lakini haihusishi Kima cha Agizo la Utoaji, Amana zitaanza kupata Riba, kama inavyoainishwa kwenye Tovuti, kuanzia Tarehe ya Ufunguaji Akaunti.

k. Riba ina maana ya riba kidogo inayohusika kama ilivyoainishwa kwenye Tovuti, ambayo itatokana na Mtaji kuanzia Tarehe ya Ufunguaji wa Akaunti.

l. Kipindi cha Uwekezaji ina maana ya muda uliochaguliwa na wewe, sio chini ya miezi mitatu(3) na sio zaidi ya miaka mitatu(3), kuanzia Tarehe ya Uanzaji hadi Tarehe ya Ukomavu, ambayo kwayo umewekeza fedha zako.

m. Tarehe ya ukomavu ina maana tarehe ambayo Kipindi cha Uwekezaji kinakwisha kiautomatiki na kiasi cha Ukomavu kinalipwa katika Akaunti Teule ya Benki.

n. Kima cha Ukomavu ina maana ya Mtaji na Riba iliyoingizwa kwenye Akaunti katika Kipindi cha Uwekezaji.

o. Akaunti Teule ya Benki ina maana ya akaunti ya benki ambayo uliichagua katika hatua ya maombi (kuwa ni akaunti iliyoainishwa nyuma ya fomu ya maombi iliyoandikwa kama " Akaunti Teule ya Benki") ambayo Kima cha Ukomavu kitalipwa iwapo hutachagua kuwekeza kwa kipindi cha ziada.

p. Sisi, yetu ina maana ya Benki ya Stanbic Tanzania na wewe au yako, ina maana ya mtu anayetuma maombi kwa ajili ya Akaunti, au ambaye Akaunti inafunguliwa kwa jina lake.

q. Tovoti ina maana ya tovuti yetu, ambayo inaainisha Riba inayohusika na Akaunti yako.

## 3. AKAUNTI YAKO

a. Ufunguaji wa akaunti: Akaunti yako itafunguliwa Tarehe ya Ufunguaji wa Akaunti, ambayo ni tarehe ambayo akaunti inachukuliwa kuwa hai. Unapofungua akaunti, utaridhia Masharti ya Uwekezaji, Kima cha Agizo la Utoaji kitacholipwa katika Akaunti Kipindi cha Uwekezaji na Tarehe ya Agizo la Utoaji.

b. Amana na ziada: Unaweza kufanya Amana za ziada katika Akaunti yako ya kima chochote kwa njia yoyote ifuatayo: utaratibu unaotumika, amana kwenye kaunta, benki ya kidigitali (Benki ya Intanet na USSD yaani *150*29).

c. Riba: utapata riba kwenye mtaji wako kama ilivyoainishwa kwenye Tovuti. Riba inakokotolewa kwa siku na kuingizwa katika Akaunti kila mwezi. Riba inaweza kubadilika kwa busara yetu na mabadiliko yoyote yataanza kutumika mara moja baada ya kukupatia taarifa ya awali ya maandishi ya siku thelathini (30).

d. Utoaji: utoaji wa Mtaji, iwe katika kaunta za tawi letu au katika Mashine za Ulipaji za Kiautomatiki (ATM) haitaruhusiwa kwa akaunti hii ya Kipindi Maalum cha Uwekezaji. Utaweza kutoa fedha kutegemea masharti ambayo yanatumika kwa Ufunguaji wa Akaunti

e. Mapema Unaweza kufunga Akaunti yako wakati wowote kabla ya Tarehe ya Ukomavu. Ufungaji mapema unaendana na athari ya wewe kusamehe riba iliyopatikana kwenye Akaunti. Akaunti itafungwa, na Mamlaka ya Agizo la Utoaji yatafutwa.

f. Malipo: Katika Tarehe ya Ukomavu kima cha kiasi cha Mtaji na Riba kitaingizwa kiautomatic katika Akaunti Teule ya Benki tulio nayo. Malipo yoyote ambayo yatafanywa katika benki nyingine yoyote kama itakavyoelekezwa na wewe kwa maandishi itasababisha tozo za miamala za ziada.

g. Ikiwa umeamua kwamba tuhamishe kima cha Ukomavu kwenye Akaunti yako Teule ya Benki, na uhamishaji huu hauwezekani kukamilika kutokana na sababu yoyote ile tutawasilisiliana na wewe. Endapo tutashindwa kukupata, tutawekeza upya Kima cha Ukomavu husika katika Akaunti kwa kipindi sawa na Kipindi cha Uwekezaji na endapo utawasiliana nasi tutafanya malipo yoyote au yote katika Akaunti kama ulivyotuagiza.

h. Ada, tozo na adhabu: Hakuna ada.

i. Athari ya Kodi:
Katika Tarehe ya Ukomavu, benki itatoa 10% kodi ya zuio kwenye Riba iliyopokewa kwa mujibu wa sheria za Kodi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Stanbic Bank

j. Hakuna Kadi ya Malipo ya Visa (Kadi ya ATM) itakayotolewa.

k. Salio la Akaunti: Salio la Akaunti linaweza kuangaliwa kwenye mtandao (Intaneti, USSD, STANBIC APP) na taarifa inaweza kuombwa katika matawi yetu.

l. Utatupatia taarifa zote za ziada kama tutakavyoomba kwa madhumuni ya AKaunti kadiri tutakavyoona muhimu.

m. Tunaweza kwa busara yetu kuwa na haki ya kubadilisha sehemu yoyote ya Masharti haya mara kwa mara baada ya taarifa ya maandishi ya siku thelathini 30 kutolewa kwako.

n. Sheria za Jamhuri ya Muungano Tanzania zitatumika kwenye Masharti haya.

☐ Nathibitisha kwamba nimesoma, nimeelewa na kukubali Maelezo na Masharti yaliyoambatishwa na fomu hii.

Saini ya Muombaji: ______________________________

Imetiwa saini Tarehe: ______________________________